



## TAARIFA KWA UMMA

### USHIRIKI WA TANZANIA KATIKA MAONESHU YA DUNIA YA EXPO2020 DUBAI

Dodoma, 9 Oktoba 2021

"EXPO" ni maonesho ya dunia yanayosimamiwa na Shirika la Kimataifa lijulikanalo kama *Bureau of International Exhibition (BIE)* lenye nchi wanachama 195. Maonesho haya hufanyika kila baada ya miaka mitano (5) ambapo hudumu kwa miezi sita (6), yakiwa na Kauli Mbiu ya Maonesho inayojikita kufanikisha masuala mbalimbali ya Kiuchumi na Kijamii kwa Nchi washiriki.

Mwaka 2013 Nchi ya Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu (UAE) ilichaguliwa kuwa mwenyeji wa **EXPO 2020 Dubai**. Awali Maonesho hayo yalipangwa kufanyika kuanzia tarehe 01 Oktoba 2020 hadi 31 Machi, 2021 lakini kutokana na changamoto ya Ugonjwa wa UVIKO 19 yalisogezwa mbele na yameanza rasmi tarehe 01 Oktoba, 2021 na yanatarajiwa kumalizika mwakani tarehe 31 Machi, 2022.

Tanzania ni Miongoni mwa nchi 191 zinazoshiriki Maonesho hayo. Ushiriki wa Nchi yetu unaratibiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda – Zanzibar, kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (*TanTrade*). Aidha, tunashirikiana pia na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kupitia Ubalizi wetu uliopo Abu Dhabi pamoja na wadau wengine wa Sekta Binafsi.

Kaulimbiu ya Maonesho haya ni **"Connecting Minds, Creating the Future"**, inayolenga kuzileta Nchi zote duniani pamoja katika kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili Dunia kwa sasa katika Sekta ya biashara, kilimo, nishati, madini, uchukuzi, viwanda, teknolojia, utalii, elimu, afya na huduma za kijamii.

Tanzania inashiriki katika eneo la **Mobility** lenye Kaulimbiu ndogo isemayo "**Connectivity, Tanzania Ready for Take Off**" ambayo inaonesha juhudi za Serikali katika kuanzisha na kuendeleza miradi ya miundombinu inayoiunganisha nchi yetu na bara la Afrika na Dunia kwa ujumla.

Pamoja na mambo mengine, Tanzania inatangaza miradi ya kimkakati kama vile mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), Reli ya Kisasa (SGR), Upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Ujenzi wa Viwanja vya Ndege na uimarishaji wa Usafiri wa Anga. Miradi hiyo ni kivutio na kichocheo cha ukuaji wa biashara na uwekezaji hususan katika Sekta za Kilimo na Viwanda.

Kadhalika, nchi yetu inatarajia kutumia fursa hii kubwa kushirikiana na Sekta Binafsi kutangaza na kutafuta masoko ya uhakika na endelevu ya bidhaa zitokanazo na mazao ya kimkakati kama vile kahawa, korosho, chai, mkonge, karafuu, viungo, bidhaa za ngozi pamoja na bidhaa nyingine zinazokidhi mahitaji ya soko la kimataifa.


Aidha, kutokana na changamoto ya UVIKO-19, waandaaji wa EXPO 2020 Dubai wanahamasisha Wafanyabiashara duniani kote kutumia fursa ya soko mtandao lililoanzishwa katika maonesho hayo (**World Market Souq**). Mtandao huo hauna tofauti sana na mitandao maarufu duniani kama vile Alibaba na Amazon pamoja na mtandao wa hapa nchini wa posta e-shop.

Napenda kutumia fursa hii adhimu kuwajulisha na kuwaalika wadau wa Sekta Binafsi na Wafanyabiashara wote wa Tanzania kuhusu fursa ya kushiriki Maonesho hayo kupitia programu mbalimbali ambazo zimeandaliwa ikiwemo ziara za kujifunza na Mikutano ya Kibiashara (B2B) inayojikita katika sekta za uwekezaji wa miundombinu, teknolojia, mipango miji na vijiji, elimu, ufundi na ubunifu, mifumo ya ufundishaji, fursa za utalii (hoteli, uwindaji, michezo, mazingira na fukwe), usafirishaji na mawasiliano, kilimo, uongezaji thamani wa mazao, nk.

Manufaa ya kushiriki katika Maonesho hayo kwa Taifa letu ni makubwa sana ikiwemo kuvutia na kushawishi upatikanaji wa mitaji katika miradi mbalimbali ya kimaendeleo pamoja na kupata wabia wa uwekezaji

watacaoendeleza sekta mbalimbali za kiuchumi hususan Kilimo na Viwanda. Vilevile Maonesho hayo yanatoa fursa kwa Makampuni kujitangaza na kunadi bidhaa na huduma zinazozalishwa hapa nchini ili kupata masoko ya uhakika kimataifa. Aidha, Maonesho hayo pia yatatuwezesha kuvutia zaidi watalii kutembelea vivutio mbalimbali vilivyopo nchini na kujifunza utamaduni na desturi za Kitanzania. Hayo yote yanatarajia kujenga na kuimarisha mahusiano ya kibiashara, kiuchumi na kijamii kati ya Sekta Binafsi ya Tanzania na Sekta Binafsi kutoka nchi nyingine zinazoshiriki.

Kwa maelezo ya namna ya kushiriki katika maonesho haya kupitia Programu mbalimbali zilizopangwa tafadhali tembelea Tovuti ya TanTrade ([www.tantrade.go.tz](http://www.tantrade.go.tz)) au wasiliana na TanTrade kupitia barua pepe: [info@tantrade.go.tz](mailto:info@tantrade.go.tz) au kwa Simu: +255715988299/717478806.



Imetolewa na:

Prof. Kitila A. Mkumbo (Mb)  
**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA**